Mwananchi tambua haki zako...

Ikiwa unaamini hujatendewa haki, toa taarifa **Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora** kupitia ujumbe wa simu ya kiganjani kwenda **Na. 0754 460 259** ukianza na neno *TAARIFA* ikifuatiwa na malalamiko lako.

Mfano: TAARIFA mimi ni mjamzito nimenyimwa huduma katika hospitali ya... kwa kuwa sikuwa na fedha za matibabu (taja jina la hospitali na namba za simu kama zipo), kisha tuma ujumbe wako kwenda **Na. 0754 460 259.**

Kumbuka: Maafisa wa Tume watawasiliana nawe kupitia namba ya simu uliyotumia kutuma ujumbe wa malalamiko yako. Endapo malalamiko yako yataanza kuchunguzwa utapewa namba maalumu ya Kumbukumbu utakayotumia kufuatilia lalamiko lako.

Jinsi ya kufuatilia malalamiko yako Tume: Tuma namba yako ya Kumbukumbu kwenda **Na. 0754 460 259** ukianza na neno STATUS. **Mfano: STATUS 13024.**

Kimetayarishwa na:

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli,
S. L. P 2643, DAR ES SALAAM/Tanzania
Simu: +255 22 2135747/8;
B/Pepe: chragg@chragg.go.tz

Kimefadhiliwa na:

Swedish Program for ICT in Developing regions (Spider)
Sedish International Development Agency (SIDA)
Legal Sectoral Reform Program(LSRP)

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

SASA UNAWEZA KU-WASILISHA MALALAMIKO YAKO MBELE YA TUME KWA NJIA YA UJUMBE WA SIMU YA KIGANJANI

MWANANCHI TAMBUA HAKI ZAKO...

HAKI ZA WANAFUNZI MASHULENI NA VYUONI

1. Je, umenyanyaswa kijinsia shuleni au chuoni?
2. Je, mnapigwa viboko vingi shuleni bila kufuata sheria ya utoaji wa adhabu hiyo?
3. Je, ukiwa shuleni au chuoni umenyanyaswa bila sababu yoyote?
4. Je, shuleni/chuoni unakosa au mnakosa mahitaji muhimu, kama vile maji safi, chakula, matibabu n.k?
5. Je, uongozi unawapatia uhuru wa kuabudu muwapo shuleni/chuoni?
6. Je, mnapata haki za kupata taarifa mbalimbali kupitia TV, Radio au magazeti hapo shuleni/chuoni?
7. Je, mnapata muda wa michezo hapo shuleni/chuoni?
8. Je, mnapata muda wa kuwasiliana na wazazi au ndugu hapo shuleni?

Ni haki yako kupata elimu bora

DAI HAKI YAKO, NA TIMIZA WAJIBU WAKO!

HAKI ZA WANANCHI KATIKA MAENEO MBALIMBALI

1. Je, Mtendaji wa kijiji au kata au tarafa amekufungia ofisini kwa muda zaidi ya masaa 24?
2. Je, umewahi kunyang'anywa kitu chochote na Mtendaji wa kata, kijiji au mgambo wa jiji kinyume na sheria?
3. Je, umewahi kupigwa na viongozi wa Serikali au kiongozi yeyote mwenye mamlaka kwenye taasisi?
4. Je, hujalipwa fidia kwa mali yako halali iliyochukuliwa na Serikali au Mwekezaji kwa shughuli maalum?
5. Je, umecheleweshewa mirathi yako baada ya kufuata taratibu husika zote?
6. Je, umekopwa mazao yako kwa muda mrefu bila kulipwa fedha stahiki?
7. Je, umehamishwa kijijini na uongozi wa kijiji kwa sababu zisizokuwa za kisheria?
8. Je, kuna mtoto, mwanamke, mtu mwenye ulemavu anateswa na wazazi/walezi, mwenza wake, ndugu au mtu yeyote?

Endapo utaona mambo ambayo yanavunja haki hizi chukua hatua!
TIMIZA WAJIBU WAKO NA
DAI HAKI YAKO

HAKI ZA WAFANYAKAZI

1. Je, umewahi kunyanyaswa kijinsia kazini?
2. Je, umewahi kunyimwa mshahara bila sababu yoyote?
3. Je, umekatwa mshahara wako bila sababu ya msingi ya kiutumishi?
4. Je, wakuu wako wa kazi hawajakupandisha cheo bila sababu za msingi za kiutumishi?
5. Je, umesimamishwa kazi bila sababu za msingi za kiutumishi?
6. Je, umefukuzwa kazi bila taratibu za kiutumishi kufuatwa?
7. Je, umefuatilia mafao yako ya kustaafu kwa muda

Ni haki yako kufanya kazi na kulipwa ujira wa haki.

DAI HAKI YAKO, USIACHE IKAPOTEA!

HAKI ZAKO UWAPO MIKONONI MWA VYOMBO VYA DOLA

1. Je, askari polisi amekukamata na kukufungia mahabusu kwa zaidi ya saa 24 bila kukufungulia mashtaka?
2. Je, jamaa yako amefariki akiwa mikononi mwa polisi baada ya kukamatwa akiwa na afya njema?
3. Je, jamaa yako amekamatwa na polisi na hujuwi aliko-pelekwa?
4. Je, polisi amekukamata bila ya kukuambia kosa lako?
5. Je, polisi amekunyang'anya kitu chochote halali bila kutoa sababu ya kuchukua kitu hicho?
6. Je, umekamatwa na kushtakiwa isivyo halali?
7. Je, askari wamekupiga au wamempiga risasi ndugu au mtu yeyote akiwa ameshikiliwa?

Haki zako haziondolewi uwapo mikononi mwa vyombo vya dola.

DAI HAKI YAKO, NA TIMIZA WAJIBU WAKO!

HAKI YA KUPATA HUDUMA BORA YA AFYA

1. Je, unajua unastahili kupata huduma bora ya afya bila kujali jinsia, dini, kabila, taifa au tabaka lako?
2. Je, unafahamu unastahili kuheshimiwa na kuthaminiwa na watoa huduma ya afya?
3. Je, unafahamu kuwa unastahili kutobugudhiwa na kwamba una uhuru wa kuamua mambo yako binafsi?
4. Je, umewahi kutozwa gharama kwa magonjwa ambayo yameondolewa katika orodha ya kulipiwa – mfano UKIMWI, Saratani, TB?
5. Je, umewahi kufika hospitalini/ kituo cha afya ukacheleweshwa kupata huduma bila sababu za msingi?
6. Je, wewe au mgonjwa wako amedhalilishwa kwa lugha zinazokwaza au za matusi kituo cha afya/ hospitali?
7. Je, una malalamiko ambayo umefikisha mbele ya uongozi wa hospitali/ kituo cha afya lakini hayakufanyiwa kazi?
8. Je, unapewa vitisho ili usichukue hatua ya kutoa taarifa ya kero/ lalamiko lako mbele ya mamlaka husika au vyombo vya sheria kufuatia huduma au lugha mbaya iliyotolewa na wauguzi wa hospitali au kituo cha afya?
9. Je, umefika hospitali/kituo cha afya na hukuwakuta wahudumu/manesi/madaktari wakati ni muda wao wa kuwa kazini?

Ni haki yako kupata huduma bora za afya.

DAI HAKI YAKO, AFYA HAINA MBADALA!